# MPANGO WA UWEZESHAJI WA TEKNOLOJIA ZA KILIMO ZA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI TANZANIA

## Mfumo wa Sera ya Makazi Mapya

Rasimu ya Mwisho

**MUHTASARI RASMI**


**Imewasilishwa na:**

**CRDB BANK PLC**
**Makao Makuu: Mtaa wa Azikiwe**
**S.L.P 268, Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: +255 (0)222117441-7**
**Nukushi +255 (0) 222116714**
**Barua pepe: info@crdbbank.com**
**Tovuti: www.crdbbank.co.tz**



***June, 2021***

# MUHTASARI RASMI WA KIUFUNDI

CRDB Bank PLC ni Kampuni iliyo binafsishwa inayoongoza kwa kutoa huduma za kifedha yenye Makao Makuu yake jijini Dar es Salaam katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ina shughuli zake Burundi. Benki ya CRDB ilianzishwa mnamo mwaka 1947 kama Benki ya Ardhi ya Tanganyika na baadaye kuwa Benki ya Maendeleo Vijijini Tanzania, na baadae kuwa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (CRDB). Benki ya CRDB inatoa mikopo ya muda mfupi, kati na muda mrefu, mtaji na dhamana kwa sekta mbalimbali, nyingi zinakabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi. CRDB inahodhi sehemu kubwa ya mikopo inayotolewa katika sekta mbalimbali ambayo pia inachangia kufanikisha kufikia malengo ya Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa juu ya Mabadiliko ya Tabia ya nchi na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Benki ya CRDB iliidhinishwa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund) mnamo Novemba 2019 kwa lengo la kusaidia Serikali na Watu wa Tanzania kuwezeshaji kupatikana kwa rasilimali za kimataifa kusaidia juhudi za Kitaifa za kushughulikia mabadiliko ya tabia nchi kupitia usimamizi wa miradi endelevu yenye kutoa nafuu kwa uchumi kupitia sekta ya benki.

Sekta ya kilimo ni moja wapo kati ya sekta zilizopo kwenye mazingira magumu ya kuathiriwa zaidi na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi katika muktadha wa Tanzania. Kwa hali halisi, Benki ya CRDB kwenye utoaji wa mikopo inawakilisha takribani asilimia 50% ya jumla ya mikopo inayotolewa na benki za biashara katika JMT kwa sekta ya kilimo. Mabadiliko ya tabia nchi yanaonyesha mlolongo wa hatari ya kupoteza mapato kwa waendeshaji wa shamba, kuzorota kwa mizania ya Benki na kupunguza uwezo wa ukuaji wa uchumina mtazamo wa jumla wa maendeleo ya nchi. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya kilimo kwa uchumi wa kitaifa na maendeleo ya kijamii, Tanzania lazima isimamie vyema athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu wa mazingira ili kuhakikisha uzalishaji wa muda mrefu wa sekta ya kilimo. Mabadiliko kwa ajili ya maendeleo ya kilimo cha Tanzania yanahitaji kutoka kwenye kilimo cha mazoea na inahitajika mbinu mbadala ikiwa ni pamoja na ugawaji wa maji kupitia umwagiliaji wa kisasa na kuboresha usimamizi wa maji na ardhi. Mbinu bora za kilimo za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi pia zinapashwa kufuatilia athari zozote hasi ambazo zinaweza kusababishwa kutotumia mbinu sahihi za kukabiliana na mabadilko ya tabia nchi kama vile mbinu zinazoongeza uzalishaji wa gesi chafu unaohusiana na mtindo wa sasa wa mabadiliko ya kilimo unaongozwa na vitu kama kuongezeka kwa utumiaji mwingi wa pembejeo kwa eneo la ardhi, utumiaji wa mitambo na kulima ardhi mpya zaidi.Ili kuondoa matatizo katiika uzalishaji wa mazao na kulinda usalama wa chakula, usimamizi thabiti wa changamoto za mabadiliko ya tabia nchi na kuongeza uwekezaji katika kukabiliana na mabadiliko kunahitajika ili kukuza wigo wa CRDB kutoa mikopo katika sekta ya kilimo ili kutoa matokeo chanya kwa mapato ya wakulima na kwa jili ya maendeleo ya Taifa.

Mpango uliopendekezwa wa " Mpango wa Uwezeshaji wa Teknolojia za Kilimo za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania (MUTKKMTT)" utaiwezesha Benki ya CRDB kuendeleza mifumo ya kifedha ya ubunifu wenye tija kupitia kwenye teknolojia ambazo ni: i) zinazofaa zaidi kwa mazingira ya hapa nchini, ii) ii) zinazoweza kwa ufanisi kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi za sasa na baadae ili kuhakikisha kuongezeka kwa mavuno ya mazao ya kilimo na iii) zinazoonyesha mahitaji ya makubwa ya soko na uwezekano mkubwa wa kuongeza mapato. Lengo kuu la mpango huo ni kuhakikisha uimara wa Kilimo cha Tanzania na wakati huo kuongeza uzalishaji wenye tija na kupunguza uzalishaji wa hewa chafu na athari zingine mbaya za mazingira.

Miradi midogo inayopendekezwa chini ya MUTKKMTT itafanyika kwenye mashamba yaliyomilikiwa tayari au kwenye ardhi na maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za kilimo bila kuwa na haja au mahitaji kidogo ya kuhamisha watu kwenda kwenye makazi mapya na bila umuhimu mkubwa wa uhamishaji wa shughuli

za kiuchumi. Kabla ya utekelezaji wa shughuli za mpango huu, kutakuwa na utoaji wa taarifa wa mapema kwa wadau ambao kwa njia moja au nyingine wanaweza kuathiriwa na mpango huu ili kupunguza athari hasi ya mpango kwa jamii ya wenyeji na wa kiasili, ardhi na maisha yao kwa ujumla.. Mpango huu utahakikisha kwamba hauvurugi maisha ya watu wa kiasili karibu na maeneo ya mpango kwa kuheshimu watumiaji wa ardhi waliopo ambao wana maisha tofauti na kilimo. Itahakikisha zaidi kuwa mfumo wa maarifa asilia umejumuishwa katika teknolojia ya kisasa na haki za jamii tofauti zinaheshimiwa. Hatahivyo, katika hatua hii ya kukuza MUTKKMTT, eneo halisi, ukubwa, na kiwango cha miradi midogo haijulikani, ilionekana kuwa inafaa kuandaa Mfumo wa Sera ya Makazi Mapya (MSMM) kuongoza utekelezaji wa Mpango huu. MSMM imeandaliwa kwa sababu MUTKKMTT itasaidia miradi mbali mbali, ambayo inaweza kuhitaji upatikanaji kwa ardhi ambayo inaweza kusababisha wakazi kulazimika kutafuta makazi mapya bila kukusudia na / au kusababisha kuwepo na vizuizi juu yaupatikanaji wa rasilimali au maisha. Hii ni kwa sababu sio wote waendelezaji wa miradi midogo midogo watakuwa tayari wameendeleza maeneo yao ya shamba au kuwa na sehemu ya ardhi iliyotengwa kwa kilimo. MUTKKMTT inaweza kuhusishwa katika upatikanaji wa ardhi inayohitajika kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa miundo mbinu ya uhifadhi wa mazao au maji, ufungaji wa mifumo ya kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya jua, uzalishaji viuatilifu ambavyo si vya kikemikali au upanuzi wa mifereji ya umwagiliaji. Kwa kuzingatia hii, kati ya waendelezaji wa miradi watatumia zaidi MSMM hii.

MSMM itatumiwa kuchanganua miradi yote midogo itakayo pendekezwa chini ya MUTKKMTT na kuona kama inaweza kusababisha uchukuaji wa ardhi na kutoa taratibu zote zinazofaa kufuata katika kupunguza uwezekano wa kusababisha shuruti ya kuhamishia watu kwenye makazi mapya. Wakati wa utekelezaji wa shughuli ndogo ndogo za mpangoi, inapohitajika, Mipango ya Utekelezaji wa Makazi Mapya (MUMM) uitatengenezwa ili kushughulikia athari maalum, hatua za kupunguza, na masuala ya fidia. MUMM zitakuwa maalum kwa miradi midogo midogo

Mfumo wa Sera ya Makazi Mapya unaweka tu kanuni za kuhamisha makazi na utoaji wa fidia, mipangilio ya Kampuni na vigezo vya ubunifui vitakavyotumiwa kwa MUTKKMTT ambavyo vitatayarishwa wakati wa utekelezaji wa mpango kwa kufuata sheria za Tanzania na Sera ya Utendaji ya GCF ya Makazi Mapya ya Lazima. Tathmini ya athari zinazoweza kupatikana katika upatikanaji wa ardhi, na utambuaji wa vikundi / watu walioathiriwa, utafanywa kwa njia ya ushirikishwa wa wadau wote kwa msisitizo maalum kwa jamii zilizoathiriwa hasaa vikundi vilivyo katika mazingira hatarishi zaidi.

MUMM za mradi mdogo baadaye tatayarishwa sambamba na mfumo huu wa sera na utawasilishwa kwa ajili ya Benki kutoa idhini baada ya taarifa maalum ya mpango kupatikana. Jitihada zitatumika ili kupunguza mahitaji ya makazi mapya katika hatua ya kusanifu miradi midogo. Tathmini na ufuatiliaji vitakuwa vitu vya msingi katika Mpango wa Utekelezaji wa Makazi Mapya. Mipangilio ya ufuatiliaji itaingizwa kwenye mpango mzima wa ufuatiliaji wa MUTKKMTT, ambayo itakuwa kupitia Kitengo cha Fedha Endelevu (KFE) cha CRDB. Kufuatilia taratibu na viwango vya fidia ambavyo vinaweza kuhitaji marekebisho KFE itafanya marekebisho hayo, ikitumia maoni kutoka kwa viashiria vinavyofuatiliwa na waendelezaji wa miradi midogo (yaani walengwa) ili kubaini ikiwa malengo yanatimizwa, na utaratibu wa malalamiko kutoka kwenye jamii ya eneo husika kuelezea kutoridhika kuhusu ulipaji  wa fidia na makazi mapya.